



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**KIKAO CHA ISHIRINI NA MOJA**

**1 JULAI, 2010**



## **ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

### **MKUTANO WA ISHIRINI**

**KIKAO CHA ISHIRINI NA MOJA – TAREHE 1 JULAI, 2010**

#### **I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

##### **WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

##### **MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA NA BIASHARA:**

Taarifa ya Kamati ya Viwanda na Biashara kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda,

Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI  
KUHUSU WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA  
NA MASOKO**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

**III. MASWALI YA KAWAIDA:**

**OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:**

**150. MHESHIMIWA RICHARD MGANGA  
NDASSA (SUMVE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utawala Bora:- Katika awamu ya kwanza **TASAF ONE** imefanya vizuri kukamilisha miradi yake yote kwenye Wilaya arobaini zilizopendekezwa na kuwafanya wafadhili kuja na awamu nyingine ya **TASAF TWO** iliyokusudia kuwa na miradi nchi nzima lakini kutokana na miradi mingi iliyobuniwa na wananchi haikuwezekana kukamilika yote na kama imekamilika haitoi huduma katika ukamilifu wote:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kushirikiana na wadau wetu wa maendeleo ili kuikamilisha miradi hiyo.

**151. MHESHIMIWA FATMA MUSSA MAGHIMBI (CHAKECHAKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utawala Bora:- Baadhi ya Viongozi wakubwa wa nchi wanakiuka Sheria ya Maadili:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba, iko haja sasa ya kutoa mafunzo kwa

Waheshimiwa Wabunge juu ya Sheria ya Maadili;

- (b) Kabla ya kutoa mafunzo hayo; Je, Serikali haioni kuwa, ni wakati muafaka sasa wa kumpatia kila Mbunge nakala ya Sheria hiyo.

## **WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

### **152. MHESHIMIWA MGANA IZUMBE MSINDAI (IRAMBA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Sasa hivi Watanzania wengi hasa wa vijijini hawapati maji kwa matumizi yao ya kawaida na wakati wa masika hasa kwenye Mikoa yapo makorongo na mito ambayo hujaa maji ambayo huishia kwenye maeneo ambayo hayana watu:-

- (a) Je, Serikali haioni kwamba ni busara kukinga maji hayo yasipotee ili yatumike kwa manufaa ya watu wetu;

(b) Je, Serikali haioni kuwa ni vema baada ya kuyakinga, maji hayo yakawa mengi ndipo sasa ifanye utaratibu wa kuyasambaza kwenye maeneo yote yanayohitaji maji hayo.

**WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

**153. MHESHIMIWA GAUDENCE CASSIAN  
KAYOMBO: (MBINGA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika:- Serikali iliahidi kuwalipa wakulima waliokopwa na Vyama vya Ushirika vya Wilaya au Mikoa na imeanza kutekeleza azma hiyo:-

Je, kwa nini Serikali haijawalipa wakulima waliokopwa na Chama cha Ushirika Wilayani Mbinga (MBICU) ambacho kilifilisiwa tangu miaka ya 90.

**WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

**154. MHESHIMIWA BENITO WILLIAM  
MALANGALILA (MUFINDI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Sasa ni miaka zaidi ya kumi na

nne (14) umeme umepita juu ya nyumba za wananchi wa kijiji cha Mninga, na ni miaka zaidi ya sita (6) umeme umepita juu ya kijiji cha Kihanga; na tathmini za gharama za kuingiza umeme katika vijiji hivyo viwili haifiki hata sh. milioni 150:-

- (a) Je, ni sababu gani za ukweli zinazosababisha wananchi hao wasipatiwe umeme kwa muda wote huo;
- (b) Je, Serikali inaelewa kuwa, wananchi hao ndio waliotoa ardhi yao kwa mwekezaji anayezalisha nguzo za kusambazia umeme sehemu nyingi za ndani na nje ya nchi.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

##### **WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:**

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

**DODOMA  
1 JULAI, 2010**

**DKT. T.D. KASHILILAH  
KATIBU WA BUNGE**